

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA BUNDA (BUNDA WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

#### Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-016-2018/2019

Mnamo tarehe 15 Oktoba 2018 Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Bunda (Bunda WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

#### Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Mabadiliko (%)	Bei Zinazopendekezwa				
	2017/18		2018/19	Mabadi liko (%)	2019/20	Mabadi liko (%)	2020/21
Majumbani	800	212%	2,496	5%	2,624	1%	2,650
Taasisi	1,200	212%	3,744	5%	3,936	1%	3,975
Biashara	1,200	212%	3,744	5%	3,936	1%	3,975
Viwanda	-	-	5,000	0%	5,000	0%	5,000
Magati	1,200	212%	3,744	5%	3,936	1%	3,975
Ujenzi	-	-	4,000	0%	4,000	0%	4,000
Kunyweshwa Mifugo	-	-	3,744	5%	3,936	1%	3,975

#### Jedwali Na.2: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	1,000	Kuondoa Tozo ya Huduma kwa Wateja Wote		
Taasisi	1,000			
Biashara	1,000			
Magati	1,000			

**Jedwali Na.3: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)**

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	32,000	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho		
Taasisi	42,500			
Biashara	42,500			
Viwanda	-			
Magati	-			
Ujenzi	-			
Kunywesha Mifugo	-			

**Jedwali Na.4: Ada za Sasa na Zinzopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)**

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinzopendekezwa					
	2017/18	Mabadi liko(%)	2018/19	Mabadi liko(%)	2019/20	Mabadi liko(%)	2020/21
Majumbani	10,500	90%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Taasisi	11,000	218%	35,000	0%	35,000	0%	35,000
Biashara	11,000	173%	30,000	0%	30,000	0%	30,000
Viwanda	-	-	35,000	0%	35,000	0%	35,000
Magati	11,000	82%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Ujenzi	-	-	35,000	0%	35,000	0%	35,000
Kunywesha Mifugo	-	-	20,000	0%	20,000	0%	20,000

**Jedwali Na. 5: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kupima Umadhubuti wa Dira za Maji (Shilingi kwa Upimaji)**

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	-	TZS 5,000 kwa kila Upimaji		
Taasisi	-			
Biashara	-			
Viwanda	-			
Magati	-			
Ujenzi	-			
Kunywesha Mifugo	-			

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bunda, sababu kuu ya kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni uhitaji wa kulipa gharama za uendeshaji na matengenezo, gharama za ukarabati na ununuzi wa vifaa, gharama za umeme na tozo zilizopo kisheria.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumanne, tarehe 27 Novemba 2018 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda** uliopo Bunda Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Bunda, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 3 Disemba 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA ZIWA, GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF; BARABARA YA KENYATTA, MWANZA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUNDA**

**Imetolewa na:**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**  
**(EWURA)**

**8 Novemba 2018**